HALIUZWI

# Jarida la NEMC

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 015 | APRILI - JUNI, 2024

# NEMC YAFANIKISHA KONGAMANO LA MAZINGIRA KATIKA KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA JNICC JIJINI DAR ES SALAAM




Ndani:

- NAIBU WAZIRI MKUU MHE. DKT. DOTTO BITEKO AHIMIZA SUALA LA UHIFADHI WA MAZINGIRA
- MAKAMU WA RAIS DKT. PHILIP ISDORY MPANGO AONGOZA ZOEZI LA USAFI SOKO LA ILALA
- ELIMU YA MATUMIZI SALAMA YA ZEBAKI YAWAFIKIA WACHIMBAJI WADOGO TAKRIBANI 600 MKOA WA MARA

# YALIYOMO


03 NEMC YAFANIKISHA KONGAMANO LA MAZINGIRA KATIKA KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA JNICC JIJINI DAR ES SALAAM

04 NAIBU WAZIRI MKUU MHE. DKT. DOTTO BITEKO AHIMIZA SUALA LA UHIFADHI WA MAZINGIRA.

06 NEMC KUKAGUA MIRADI YA MAENDELEO KUJIRIDHISHA UHIFADHI WA MAZINGIRA KWA MUJIBU WA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

07 NEMC YASISITIZA WADAU KUFANYA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA KABLA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI

08 MKURUGENZI MKUU NEMC DKT. IMMACULATE SWARE SEMESI AZUNGUMZA WAKATI WA UFUNGUZI WA WARSHA YA MABADILIKO YA TABIANCHI DODOMA

08 NEMC, GCLA YAENDESHA MAFUNZO YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA KEMIKALI KWA WACHIMBAJI WADOGO MAMLAKA YA MJI MDOGO MAKONGOLOSI WILAYANI CHUNYA

09 MAKAMU WA RAIS DKT. PHILIP ISDORY MPANGO AONGOZA ZOEZI LA USAFI SOKO LA ILALA

09 NEMC NA TIMU YA UFUATILIAJI MIRADI KUTOKA MFUKO WA KUHIMILI MABADILIKO YA TABIANCHI YATUA MANYONI

10 NEMC KUFANYA MAPITIO YA ATHARI ZA MAZINGIRA KWENYE MIRADI NCHI NZIMA

11 NEMC YATOA SIKU TISINI (90) UJENZI WA MIUNDOMBINU YA KUTEKETEZA TAKA HATARISHI KATIKA TAASISI ZINAZOTOA HUDUMA ZA AFYA NCHINI

11 NEMC NA TIMU YA UFUATILIAJI MIRADI KUTOKA MFUKO WA KUHIMILI MABADILIKO YA TABIANCHI YATUA MANYONI

12 MAKAMU WA RAIS DKT. PHILIP ISDORY MPANGO AZINDUA CHAPISHO LA UTAFITI WA HALI YA MAZINGIRA YA BAHARI NA PWANI

14 NEMC YAPONGEZWA KWA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MABADILIKO YA TABIANCHI

15 NEMC, GCLA YAENDESHA MAFUNZO YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA KEMIKALI KWA MAAFISA FORODHA MPAKA WA SIRARI

16 ELIMU YA MATUMIZI SALAMA YA ZEBAKI YAWAFIKIA WACHIMBAJI WADOGO TAKRIBANI 600 MKOA WA MARA

17 ELIMU YA MATUMIZI SALAMA YA ZEBAKI YATUA KIJIJI CHA RWAMGASA-GEITA

18 NEMC YAPIGA KAMBI KANDA YA ZIWA, ELIMU YA MATUMIZI SALAMA YA ZEBAKI YATOLEWA

19 WANACHAMA WA TASCC KUTOKA SHULE YA ST. MARYGORETI WAPATIWA ELIMU YA MAZINGIRA

20 MAAFISA FORODHA MPAKA WA TUNDUMA NA MAAFISA MAZINGIRA WA MIKOA YA SONGWE NA MBEYA WAPATIWA MIONGOZO NA ELIMU YA MATUMIZI SALAMA YA ZEBAKI

21 ELIMU YA UTUNZAJI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA YATOLEWA BANDA LA NEMC MAONESHO YA MBEYA CITY EXPO 2024

22 NEMC YASHIRIKI MAADHIMISHO YA MAZINGIRA DUNIANI YALIYOFANYIKA KITAIFA JIJINI DODOMA KATIKA VIWANJA VYA JAKAYA KIKWETE CONVENTION CENTER

24 NEMC YAWAONYA WAUZAJI CHUMA CHAKAVU KUHUSIANA NA ATHARI KIAFYA

25 WAZIRI JAFO MGENI RASMI HAFLA YA KUWAAGA WASTAAFU NEMC

26 WAZIRI JAFO AWATAKA MAAFISA MAZINGIRA NCHINI KUSIMAMIA SHERIA YA MAZINGIRA KWENYE MAENEO YAO

27 NEMC KUSHIRIKIANA NA PEW NA WETLANDS INTERNATIONAL KATIKA UHIFADHI WA MAENEO YA FUKWE ZA BAHARI

27 MIZAMBARAU 3000 YAPANDWA MTO TEGETA


## UTANGULIZI

### BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria hiyo Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira; na
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.


**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti:**
**Dkt. Menan Jangu**

**Mhariri Mkuu:**
**Irene John**

**Wachangiaji:**
Dalia Charles
Dkt. Rose Mtui
Martha Kawishe
Tajiri Kihemba
Nana Elias
Boniphace Kyaruzi

**Msanifu Michoro:**
Blasius Haule

# NEMC YAFANIKISHA KONGAMANO LA MAZINGIRA KATIKA KITUO CHA MIKUTANO CHA KIMATAIFA CHA JNICC JIJINI DAR ES SALAAM




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wakati wa uzinduzi wa chapisho la utafiti wa hali ya mazingira ya Pwani na Bahari Tanzania Bara katika Kongamano la Mazingira lililofanyika katika kituo cha mikutano cha Kimataifa JNICC Jijini Dar es Salaam.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuelekea maadhimisho ya wiki ya mazingira duniani, limeratibu kongamano la kitaifa la Mazingira lililohusisha wadau mbalimbali kwa lengo la kujadiliana namna bora ya kuhifadhi na kusimamia Mazingira kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake, hafla iliyofanyika katika kituo cha kimataifa cha JNICC Jijini Dar es Salaam tarehe 31 Mei, mwaka huu. Kongamano hilo lilikuwa ni sehemu ya kuadhimisha wiki ya Mazingira Duniani inayofanyika tarehe 1 hadi 5 Juni ya kila mwaka ambapo Mgeni rasmi alikua Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdory Mpango.

Lengo la kongamano hilo lilikuwa ni kuunga mkono jitihada za Serikali katika **mpango kabambe wa kitaifa wa hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa mwaka (2022 hadi 2032)** na pia ni katika kutekeleza majukumu ya Baraza ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake kuelekea wiki ya Mazingira Duniani inayofanyika kila tarehe 05 ya mwezi Juni kila mwaka, ambapo Tanzania huungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku ya mazingira. Siku hii huadhimishwa na mada tofauti zinazolenga kushughulikia au kuongeza ufahamu juu ya jambo fulani mahususi. Kaulimbiu ya Kimataifa ya mwaka huu ilikuwa ni "Urejeshaji wa Ardhi, ustahimilivu wa hali ya jangwa na Ukame" ambapo kongamano hilo lililofunguliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Philip Isdory Mpango liliendesha mada zilizojikita katika kuimarisha masuala ya mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa. Mada hizo zilibeba malengo mahususi katika maeneo yafuatayo:

a) Kukuza uelewa kuhusu changamoto za kimazingira tunazokabiliana nazo kama nchi;

b) Kupatikana ufumbuzi wa changamoto za kimazingira zilizoainishwa kwenye Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 -2032):

- Kukuza uelewa wa masuala ya mazingira na maendeleo endelevu;
- Kutoa fursa ya kubadilishana uelewa, taaluma na uzoefu kwa wadau ikiwa ni pamoja na sekta binafsi, wasimamizi wa sheria, watafiti, watunga sera, na mashirika yasiyo ya kiserikali; na
- Kutoa mapendekezo na hatua stahiki zinazopaswa kuchukuliwa na sekta mbalimbali ili kufikia maendelo endelevu.

Kadhalika, kongamano lilihusisha mijadala mbalimbali iliyozingatia vipaumbele vya kitaifa ambavyo ni:

a) Changamoto kubwa tatu za kidunia ambazo pia zinaoenekana nchini kwetu: mabadiliko ya tabia nchi; kupotea kwa bioanuai na uchafuzi wa mazingira;

b) Matumizi na nishati safi kulinda mazingira na afya ya jamii;

c) Udhibiti wa taka ngumu na suluhisho la uchafuzi wa plastiki; na

d) Wajibu wa sekta binafsi katika uhifadhi wa mazingira.

Majadiliano kwenye mada hizo yalipangwa kusaidia katika kutoa mapendekezo ya maamuzi kwenye vipaumbele na namna sahihi ya kukabiliana na changamoto za mazingira. Hivyo basi, wadau walipata fursa ya kuelezea kwa kina hali iliyopo, mifumo inayoweza kuleta mabadiliko chanya, jitihada mbalimbali zinazofanywa na wadau ikiwa ni pamoja na

Inaendelea Uk. 05

# NAIBU WAZIRI MKUU MHE. DKT. DOTTO BITEKO AHIMIZA SUALA LA UHIFADHI WA MAZINGIRA.



*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko ( wa kwanza kushoto) akiambatana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt Seleman Jafo (katikati) pamoja na viongozi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) wakifafanuliwa jambo na Afisa wa NEMC Bi. Pendo Kundya (wa kwanza kulia) alipozuru banda la NEMC Maonesho ya wiki ya Mazingira Duniani Katika Viwanja vya Jakaya Kikwete Convention Centre, Dodoma.*

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko amezitaka Wizara na Taasisi zote za Serikali kuwa na kitengo cha Mazingira na kuweka mikakati ya namna sahihi ya kuhifadhi mazingira kwa mstakabali wa maendeleo endelevu ya Taifa.

Ameitoa kauli hiyo alipozuru Banda la NEMC katika sherehe za ufunguzi wa mabanda ya maonesho ya wiki ya mazingira duniani yaliyofanyika viwanja vya Jakaya Kikwete Dodoma yenye kaulimbiu isemayo "urejeshwaji wa Ardhi, ustahimilivu wa hali ya jangwa na ukame"

Dkt. Biteko amesema nchi yetu inakumbwa na majanga ya kimazingira kutokana na kukosekana dhana ya Uhifadhi inayomtaka kila mwananchi kuwajibika ili kuepukana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Amesema "ifike mahala kila mmoja wetu awe mzalendo, ukikuta mtu anachafua vyanzo vya maji uone anatuathiri sote, ukiona mtu anakata miti hovyo uone anatuathiri sote, ukiona mtu anachimba mashimo bila kufukia uone anatuathiri sote, hivyo ndivyo dhana ya uhifadhi itajengeka."

Naye Waziri mwenye dhamana ya Mazingira Dkt.Seleman Jafo alipozungumza alisisitiza umuhimu wa matumizi ya nishati mbadala kwani ndiyo msingi imara wa kuhifadhi mazingira kwa kuepuka kukata miti hovyo.

Aidha amesisitiza umuhimu wa uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira kwa wananchi ili kuokoa mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

Hafla hiyo ya ufunguzi ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhandisi Cyprian Luhemeja, Naibu katibu Mkuu (Muungano) Bw. Abdallah Hassan Mitawi, Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Bi. Christina Mndeme, Kaimu Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais Bi. Kemilembe Mutasa, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Bi. Rosemary Senyamule, wakuu wa Wilaya, wadau wa mazingira, Taasisi za Serikali na binafsi, Mashirika ya Umma na binafsi, Wizara pamoja na viongozi wengine wa vyama na Serikali.

... Inatoka Uk. 03

## NEMC YAFANIKISHA KONGAMANO LA ...

sekta binafsi katika kusimamia na kutunza mazingira. Aidha, mijadala ilijikita kwenye suala zima la ushirikishwaji wa wadau na jamii katika kutafuta ufumbuzi wa pamoja wa kukabiliana na changamoto za mazingira.

Ikumbukwe kuwa, matatizo ya kimazingira yanatofautiana kutokana na visababishi vyake na hivyo ufumbuzi wa kila tatizo unatakiwa uendane na uhalisia, iwapo tunatarajia kuona maendeleo endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho. Baraza linaamini kuwa utoaji elimu na kukuza uelewa kwenye masuala ya mazingira kutasaidia katika kufanikisha azma ya uhifadhi endelevu wa mazingira. Hii ni kwa kuzingatia kuwepo kwa mazingira safi na salama kama nguzo muhimu kwa maendeleo ya uchumi nchini.

Vilevile kongamamno lilienga kutoa fursa kwa wadau kubadilishana uzoefu na uelewa, mbinu sahihi na kwa pamoja kufikia maamuzi ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa juu ya uzingatiaji, uendelevu na usimamizi wa mazingira katika taswira ya kikanda, kitaifa na kimataifa.

Pamoja na malengo yaliyotajwa, Baraza lilipata fursa ya kuzindua Chapisho la Hali ya Mazingira ya Pwani na Bahari ya Tanzania Bara. Chapisho hili linatoa taarifa ya hali halisi ya bioanuai, mifumo ikolojia, maliasili, mazingira na jamii. Pia kupitia chapisho hili, kwa kiasi kikubwa elimu ya utunzaji wa mazingira inakuzwa na kuongeza uelewa wa masuala ya mazingira ya pwani na bahari na kukuza uwezo wa kitaaluma na kifedha katika kukabiliana na changamoto zinazoendelea za mazingira nchini na duniani kote.

Kongamano hilo lilihudhuriwa pia na viongozi wa vyama na Serikali wakiwemo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Selemani Jafo, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mha. Cyprian Luhemeja, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NEMC Prof. Esnat Chaggu, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi

Siku ya
MAZINGIRA Duniani

na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi pamoja na wakurugenzi wastaafu wa Baraza. Kulikuwa pia na washiriki takribani 1,200 kutoka Taasisi binafsi na za Serikali, vyama vya ushirika, Viongozi wa Dini, Mabalozi wakiwakilishi wa Nchi mbalimbali hapa Tanzania, Mashirika ya Kimataifa, Wizara, Sekta mbalimbali, Watafiti kutoka vyuo vikuu, Taasisi za Tafiti, Menejimenti na Watumishi wa NEMC, Sekta na Mashirika Binafsi nchini, Mashirika ya kiraia, Wataalamu wa Mazingira (TEEA), Maafisa Mazingira kutoka Mikoa, Wilaya, Kata na Mitaa, Mashirika yasio ya Kiserikali, Wataalamu ambao walishiriki katika kuandaa Chapisho la Hali ya Mazingira ya Pwani na Bahari (SoC), wafadhili/ wawezeshaji wa Kongamano, vikundi pamoja na vyombo vya habari.



*Wadau wa Mazingira na wageni waalikwa wkifuatilia kongamano*

# NEMC KUKAGUA MIRADI YA MAENDELEO KUJIRIDHISHA UHIFADHI WA MAZINGIRA KWA MUJIBU WA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA



*Meneja wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria NEMC Bw. Hamadi Taimuru alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa mikutano wa NEMC Dar es Salaam. Kulia kwake ni Meneja Mawasiliano na Uhusiano NEMC Bi. Irene John.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeendelea na utaratibu wa kupitia miradi yote iliyopatiwa vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) ili kujiridhisha kama wamiliki wa miradi hiyo wanatekeleza matakwa ya kisheria yaliyoainishwa kwenye vyeti hivyo wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria NEMC Bw. Hamadi Taimuru alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa mikutano wa NEMC Dar es Salaam kuhusiana na mwenendo wa Utekelezaji na Uzingatiaji wa Sheria katika eneo la Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

Bw. Taimuru alisema Baraza limefikia uamuzi huo baada ya kuona miradi mingi haifuati masharti yaliyoainishwa kwenye vyeti vya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kuhakikisha kwamba Mazingira yanaendelea kutunzwa wakati wa utekelezaji wa mradi na baada ya kukamilika kwa mradi.

> ***"Tumeandaa mkakati wa kuwatembelea mmoja mmoja ili kukagua na kujiridhisha matakwa ya cheti na wao wanafanya nini kwa lengo la kuhakikisha mazingira yetu yanaendelea kuwa safi na salama na wananchi wakae katika mazingira yenye afya na hata kazi zao ziweze kwenda vizuri"***
>
> Alisema Bw. Taimuru.

Akizungumza kuhusu kaguzi za kila mwaka za mazingira Bw. Taimuru alisisitiza wawekezaji kujikagua na kuwasilisha taarifa zao Baraza ili zipitiwe na kujiridhisha kama zimezingatia masharti, huku akiwashukuru wawekezaji waliokwisha kufanya hivyo na tayari taarifa zao zimeshapitiwa na Baraza na kujibiwa kwa mujibu wa Sheria.

Katika hatua nyingine Meneja Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma (NEMC) Bi. Irene John alipozungumza alisisitiza umuhimu wa wawekezaji kuzingatia masharti ya cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kuahidi kuendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kufanya Tathimini ya Athari kwa Mazingira kabla ya kuanza miradi ili Tanzania iendelee kuwa salama kwa wageni, wenyeji, wanyama na hata vizazi vijavyo kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

# NEMC YASISITIZA WADAU KUFANYA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA KABLA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limewataka wadau wote nchini kuzingatia umuhimu wa ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya utekelezaji wa miradi kama inavyoelekezwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake ili kunusuru uharibifu wa Mazingira unaoweza kujitokeza.

Hayo yalibainishwa na Afisa Usimamizi wa Mazingira wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Bi. Gladness G. Malisa alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari juu ya umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira katika Ukumbi wa Mikutano wa Baraza uliopo Jijini Dar es Salaam.

Bi. Gladness alisema lengo la kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira ni kubaini athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi katika eneo husika.

"Lengo kuu ni kubaini athari zinazoweza kutokea kutokana na uendeshwaji wa miradi kabla ya kuanzishwa kwake ili ziweze kudhibitiwa mapema kabla hazijatokea na kuleta madhara kwa jamii" Amesema Gladness.

Akizungumzia wadau wanaopaswa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira Bi. Gladness amesema ni wawekezaji wote wa miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya Serikali na Sekta binafsi.




*Afisa Usimamizi wa Mazingira wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Bi. Gladness G. Malisa akizungumza na vyombo vya habari juu ya umuhimu wa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira katika ukumbi wa Baraza Jijini Dar es Salaam.*

"Anayetakiwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira ni mwekezaji yeyote anayetekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo Serikali, mtu binafsi, Makampuni, Taasisi au Shirika ambapo kabla ya kuanzisha mradi wowote ule ni takwa la kisheria kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira." Alisisitiza Bi. Gladness.



Naye Meneja Usajili wa Wataalamu elekezi wa Mazingira NEMC Bi. Edica Masisi alipozungumza alisema Baraza halizuii wala kuweka vikwazo kwa wawekezaji katika shughuli za maendeleo lakini ni lazima kuhakikisha shughuli za uzalishaji zinazingatia uhifadhi wa mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

Aidha, Baraza liliagiza miradi yote inayotarajiwa kuanzishwa izingatie umuhimu wa ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira kabla ya kuanzishwa na ile ambayo imesajiliwa Baraza kwa ajili ya kufanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na haijakamilika ikamilike mara moja.

## MKURUGENZI MKUU NEMC DKT. IMMACULATE SWARE SEMESI AZUNGUMZA WAKATI WA UFUNGUZI WA WARSHA YA MABADILIKO YA TABIANCHI DODOMA

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dkt. Immaculate Sware Semesi, alizungumza katika mkutano uliohusisha nchi 34 katika warsha ya mabadiliko ya tabianchi iliyofanyika Jijini Dodoma.

Akizungumza katika warsha hiyo iliyoandaliwa na ofisi yake kwa kushirikiana na Mfuko wa Kimataifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (Adoptation Fund) na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhandisi Cyprian Luhemeja pamoja na washiriki kutoka mataifa 34, alisema ni kwa lengo la kubadilishana uzoefu wa namna ya kuendeleza miradi hususani ya mabadiliko ya tabianchi na kujengeana uwezo wa namna ya kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya Tabianchi nchini Tanzania.



*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi akizungumza wakati wa ufunguzi wa warsha ya mabadiliko ya Tabianchi Jijini Dodoma.*

Alisema warsha hii iliyofanyika katika Hotel ya Best Western Dodoma itakwenda kuwa chachu kwa Taifa katika mapambano dhidi ya changamoto za mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa Mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

## NEMC, GCLA YAENDESHA MAFUNZO YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA KEMIKALI KWA WACHIMBAJI WADOGO MAMLAKA YA MJI MDOGO MAKONGOLOSI WILAYANI CHUNYA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Tume ya Madini Mkoa wa Mbeya waliendesha mafunzo ya usimamizi na udhibiti wa kemikali ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo waliopo katika Kata za Makongolosi, Bwawani na Mkola zilizopo katika Mamlaka ya mji mdogo Makongorosi Wilaya ya Chunya Mkoani Mbeya.




*Picha ya pamoja ikionesha watumishi kutoka NEMC, GCLA, Ofisi ya Madini pamoja na washiriki wa mafunzo ya matumizi ya salama ya kemikali ya zebaki kutoka Chunya.*

Mafunzo hayo yaliendeshwa kupitia Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo (EHPMP) unaoratibiwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na kufadhiliwa na Benki ya Dunia.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo Mhandisi Boniface Kyaruzi kutoka NEMC alisema wanaendesha mafunzo hayo kukumbushana wajibu uliopo kwa wachimbaji wadogo kwenye suala zima la usimamizi wa matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji hao

Alisema Serikali imefanya jitihada kubwa katika kuhakikisha madhara ya matumizi ya kemikali ya zebaki kwa wachimbaji yanadhibitiwa kwa kutekeleza matakwa ya Mkataba wa Minamata pamoja na kuwepo kwa Sheria zinazotoa miongozo ya utekelezaji wa matakwa ya mkataba huo ikiwemo Sheria ya Mazingira, Sheria ya Kemikali iliyopo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na Kanuni mahususi za zebaki kwa ajili ya kutekeleza mkataba huo.

# MAKAMU WA RAIS DKT. PHILIP ISDORY MPANGO AONGOZA ZOEZI LA USAFI SOKO LA ILALA

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Philip Isdory Mpango katika kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliyokuwa na kaulimbiu isemayo "Urejeshwaji wa ardhi, ustahimilivu wa hali ya jangwa na ukame" aliongoza wananchi wa Mkoa wa Dar es salaam katika zoezi la usafi uliofanyika Soko la Ilala.

Akiongoza zoezi hilo lililohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa vyama na Serikali, Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango alisema kuelekea siku ya mazingira duniani Juni 01, Serikali imeitenga mahususi kwaajili ya kufanya usafi Nchi nzima lengo likiwa ni kuhamasisha ari ya watanzania kutambua umuhimu wa kufanya usafi katika maeneo yao na kulifanya liwe zoezi endelevu ili kunusuru uchafuzi wa mazingira unaoambatana na uchafuzi wa hali ya hewa na magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu.

Alisema "Asanteni sana kwa kunileta eneo hili la soko, maana mlitaka kunipeleka sehemu nyingine mimi nikataka hapa kwenye wananchi wangu, nimeshuka tu hapa nikapokelewa na harufu mbaya kabisa, nikajiuliza maswali mengi, sasa namna hii siyo sawa, ni lazima kuwekwe utaratibu mzuri wa kusafisha maeneo yenye msongamano wa watu kama hivi, na sasa sisi leo tumefanya hivi ili kuwajengea wananchi wetu hulka ya kufanya usafi mara kwa mara na sio kusubiri nyakati maalumu." Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Philip Isdory Mpango akiongoza zoezi la usafi katika soko la Ilala kuelekea Siku ya Mazingira Duniani.*

> "Tarehe 05 ya mwezi wa sita kila mwaka ni Siku ya Mazingira Duniani,
>
> hivyo kama watanzania tumetenga wiki hii nzima kwa ajili ya shughuli za kimazingira na moja wapo ndio hii ya kufanya usafi ili kuhamasisha utunzaji wa Mazingira yetu"
>
> Alisema Dkt. Mpango.

Alizitaka mamlaka za Mikoa kuweka utaratibu wa kushindanisha Halmashauri masuala ya usafi ili kuleta msukumo wa kutunza na kuhifadhi Mazingira.

Katika hatua nyingine ametoa siku Saba kwa DAWASA kuhakikisha wanatatua kero ya maji yanayotiririka na kuhatarisha maisha ya wafanyabiashara katika soko hilo la Ilala.

Nae Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis amezitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kote Nchini kutekeleza Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake ili kutunza Mazingira.

Zoezi hilo la usafi lilihudhuriwa pia na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mussa Azzan Zungu, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri zote tano za Mkoa wa Dar es Salaam na wadau wote wa Mazingira katika Mkoa huo.

# NEMC KUFANYA MAPITIO YA ATHARI ZA MAZINGIRA KWENYE MIRADI NCHI NZIMA




*Afisa Mazingira Mwandamizi wa NEMC, Bw. Innocent Makomba akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonesho ya siku ya mazingira duniani yaliyofanyika jijini Dodoma*

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limejipanga kufanya mapitio ya miradi yote inayotekelezwa nchini ili kuangalia kama imefanyiwa Tathmini ya athari za mazingira katika kukabiliana na athari za kimazingira zinazotokana na shughuli za miradi hiyo.

Afisa Mazingira Mwandamizi wa NEMC, Bw. Innocent Makomba akizungumza na waandishi wa habari kwenye maonesho ya siku ya mazingira duniani yaliyofanyika jijini Dodoma, alisema lengo ni kuangalia miradi iliyofanyiwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kama inatekeleza masharti ya cheti kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake na ambayo haijafanyiwa tathmini hiyo ili ifanyiwe.

"Lengo ni kuhakikisha athari za mazingira haziharibu ardhi yetu, ustahimilivu wa hali ya jangwa na ukame, tutakachokwenda kufanya kwenye miradi yote iliyofanyiwa tathmini, ni pamoja na kuangalia masharti waliyopewa na Mheshimiwa Waziri kama yanazingatiwa,"alisema.

Alisema NEMC itaendelea kutekeleza maelekezo ya viongozi katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya mazingira ili kuhakikisha urejeshaji wa mazingira yaliyoharibiwa unafanikiwa.

"Tutahakikisha Sheria yetu inasimamiwa kikamilifu ikiwemo kufanyika kwa Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa miradi yote inayokwenda kutekelezwa,"alisema.

Kuhusu vifungashio kuchangia uchafuzi wa mazingira, Ofisa Mazingira huyo alisema NEMC itaendelea kusimamia Kanuni ya mwaka 2022 iliyoweka katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki.

"Kwa sasa tunaendelea na operesheni kwenye viwanda maana huko ndo shina lilipo, lakini pia watanzania tubadilike tunapokwenda kufanya manunuzi tubebe mifuko yetu, karatasi au vikapu vya nguo ili kuepuka kutumia vifungashio kama mifuko ya plasiki iliyokatazwa,"alisema.

Alitoa rai kwa viwanda vinavyotengeneza vifungashio hivyo kuacha mara moja na NEMC haitasita kuvichukulia hatua kwa mujibu wa Sheria.

"Vifungashio hivi vina athari maana wakati mwingine vinafungashiwa chakula cha moto, hali inayohatarisha mtu kupata saratani,"alisema.

Naye, Ofisa Mazingira Mkuu kutoka NEMC, Bi. Pendo Kundya, alipozungumza alisema katika maonesho hayo wametoa elimu kwa umma na kupokea maoni namna ya kuboresha mazingira nchini.

"Tumetoa elimu ya shughuli mbalimbali zinazofanywa na NEMC kama vile Tathmini ya Athari kwa Mazingira, tafiti zinazofanywa za mazingira, udhibiti wa kelele, mifuko ya plastiki na uzingatiaji wa Sheria ya mazingira,"alisema.

Alisisitiza wananchi kupenda mazingira na kuyatunza kwa kuwa kila mwananchi ana jukumu hilo na siyo kuiachia Serikali peke yake.

# NEMC YATOA SIKU TISINI (90) UJENZI WA MIUNDOMBINU YA KUTEKETEZA TAKA HATARISHI KATIKA TAASISI ZINAZOTOA HUDUMA ZA AFYA NCHINI

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limetoa siku tisini (90) kwa Taasisi zote nchini zinazojishughulisha na utoaji wa huduma za afya kujenga miundombinu ya kuteketeza taka hatarishi (incinerator) ili kunusuru uchafuzi wa mazingira utokanao na utupwaji holela wa taka zitokanazo na huduma za afya.

Agizo hilo lilitolewa na Meneja wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria NEMC Bw. Hamad Taimuru Kissiwa alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari katika ukumbi wa mikutano wa NEMC Dar es Salaam Mei 16 mwaka huu, kufuatia tatizo la utupaji holela wa taka zitokanazo na huduma za afya katika maeneo mbalimbali yasiyokua rasmi.

Bw.Taimuru alisema kumekuwa na uchafuzi wa mazingira utokanao na taka zitokanazo na huduma za afya ambapo taka nyingi ni zile zenye ncha kali, viungo vya mwili, vitambaa, damu mgando zinazotupwa bila utaratibu baada ya huduma hali inayohatarisha afya ya jamii na mazingira.

Bw. Taimuru alizielekeza Mamlaka za udhibiti nchini zinazoshughulikia usimamizi wa taka hatarishi zinazotokana na huduma za afya kuhakikisha wanafuata Miongozo iliyowekwa na Wizara pamoja na masharti ya Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa taka hatarishi ili kunusuru afya ya mazingira na viumbe hai.




*Meneja wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria NEMC Bw. Hamad Taimuru Kissiwa (katikati) akizungumza na vyombo vya habari katika ukumbi wa mikutano wa NEMC Dar es Salaam Mei 16 mwaka huu. Kulia kwake ni Meneja wa Kanda ya Mashariki Kaskazini Bi. Glory Kombe, na Kushoto kwake ni Meneja Mawasiliano na Uhusiano NEMC Bi. Irene John*

# NEMC NA TIMU YA UFUATILIAJI MIRADI KUTOKA MFUKO WA KUHIMILI MABADILIKO YA TABIANCHI YATUA MANYONI



*Picha ya pamoja ikionesha watumishi kutoka NEMC, Timu ya ufuatiliaji wa miradi pamoja na uongozi wa ofisi ya Wilaya ya Manyoni mara baada ya kukamilika kwa kikao.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) pamoja na Timu ya ufuatiliaji miradi (Project Monitoring Mission) kutoka mfuko wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi (Adaptation Fund) watembelea Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na kufanya Mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Manyoni juu ya mradi wa uvunaji maji kimkakati (SWAHAT) unaotekelezwa na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA).

Wakati wa mazungumzo hayo Mkuu wa Wilaya ya Manyoni Mhe. Kemirembe Lwota alilishukuru Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) pamoja na Mfuko wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kuleta mradi katika Wilaya yake na kusisitiza ushirikishwaji wa wananchi katika kutekeleza mradi huo ili uweze kuleta tija iliyokusudiwa

Naye Bi. Anastazia Tutuba Mkurugenzi wa Halmashuri ya Wilaya ya Manyoni alipopata wasaa wa kuzungumza aliushukuru ufadhili wa mfuko huo na kuahidi kuendelea na Mradi katika usimamizi mara utakapo kabidhiwa kwenye Halmashuri yake.

# MAKAMU WA RAIS DKT. PHILIP ISDORY MPANGO AZINDUA CHAPISHO LA UTAFITI WA HALI YA MAZINGIRA YA BAHARI NA PWANI




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe.Dkt. Philip Isdor Mpango (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wakati wa uzinduzi wa chapisho la utafiti wa hali ya mazingira ya Pwani na Bahari Tanzania Bara katika Kongamano la Mazingira lililofanyika katika kituo cha mikutano cha Kimataifa JNICC*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango alizindua Chapisho la utafiti wa hali ya mazingira ya Pwani na Bahari Tanzania Bara huku akiagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuangalia mapungufu ya kisheria yanayosababisha kukosa nguvu katika usimamizi wa usafi wa mazingira ili kufanyiwa marekebisho.

Akizungumza kwenye Kongamano la Mazingira lililoandaliwa na Baraza katika

> **" Tumepiga kelele za kutosha kuhusu usimamizi, utunzaji na usafi wa mazingira, NEMC nendeni mkaangalie Sheria zenu na Taasisi nyingine, mnipe mrejesho nijue tatizo ni nini"**
>
> alisema Dkt. Mpango.

kituo cha kimataifa cha mikutano cha Julius Nyerere Convention Centre (JNICC) kilichopo Jijini Dar es Salaam, Dkt. Mpango alisema miji mingi taka zimejaa kila kona na NEMC hawana meno kisheria.

Alisema kwa sasa athari za mabadiliko ya tabianchi zinachangia upotevu wa asilimia moja ya pato la Taifa na inakadiriwa ifikapo Mwaka 2030 kuna uwezekano wa kupoteza asilimia tatu ya pato la Taifa kama hatua madhubuti hazitachukuliwa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi alipozungumza alisema kongamano hilo limewakutanisha wadau mbalimbali wa mazingira kwa lengo la kujadiliana namna bora ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ili kupata mikakati ya pamoja ya kuzitambua na kushughulikia kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

"Nchi yetu na Dunia kwa ujumla inakabiliwa na changamoto za kimazingira, mfano mabadiliko ya hali ya hewa, tabianchi, upotevu wa baioanuai, uchafuzi na uharibifu wa mazingira, upungufu wa maliasili, ni ukweli unaoathiri maisha yetu ya kila siku ya afya, makuzi, mahusiano, uchumi na madhara yake yatakwenda hadi vizazi vijavyo tusiposhughulikia sasa." Alisema Dkt. Sware.

"Makubaliano ya kisayansi yapo wazi kwamba hatua za haraka na madhubuti zinahitajika ili kulinda mazingira yetu" alisema Dkt. Immaculate.

"Baraza lina jukumu la kulinda na kuhifadhi mazingira kwa mujibu wa Sheria ya mazingira namba 20 ya mwaka 2004 na limepewa jukumu la kusimamia athari za mazingira nchini zinazotokana na shughuli za kibinadamu," alisema Dkt. Immaculate.

Alisema usimamizi wa mazingira umeendelea kuhitaji mbinu mpya na za kimkakati kutokana na mabadiliko yanayoendelea kuwepo katika mifumo ya ikolojia na mbinu na teknolojia za uvunaji na uzalishaji.

Alifafanua kuwa katika kuelekea siku ya mazingira duniani Baraza liliona ni muhimu wadau kupata elimu ya mazingira.

"Tunategemea kongamano hili litakuja na njia ya kupunguza changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira na upotevu wa bioanuai," alisema Dkt. Immaculate.

Kadhalika, alisema katika kongamano hilo wadau watajadili matumizi ya nishati safi kwa Maendeleo ya nchi na jamii.

"Pia tutajadili uthibiti wa taka ngumu, plastiki na ushiriki wa sekta binafsi katika kuhifadhi mazingira, jambo jingine kupitia kongamano hili ni kuwa na jukwaa mahsusi la wadau wa mazingira nchini ili kukutana kila mwaka kuwa na mikakati yenye tija katika usimamizi wa mazingira nchini," alisema.

"NEMC inathibitisha katika kujitathmini, kujiboresha na kujiimarisha katika kushauri Serikali kwenye usimamizi wa mazingira nchini. Leo kutazinduliwa chapisho la hali ya mazingira ya Pwani na Bahari Tanzania Bara ambapo kazi hiyo ilifanyika NEMC kwa kushirikiana na Taasisi nyingine," alisema Dkt. Mpango.

Akiwasilisha maelezo kuhusu chapisho hilo, Dk. Julius Francis kutoka Chuo Kikuu Cha Dar es salaam (UDSM) alisema ni chapisho la pili kuzinduliwa katika kipindi cha mwezi mmoja na kwamba chapisho la kwanza lilihusu upande wa Zanzibar.

"Chapisho hili limeandaliwa kwa kufuata matakwa ya mkakati wa Taifa wa usimamizi wa rasilimali za Pwani na Bahari, unaotoa mchango katika uandaaji wa taarifa ya mazingira na kutimiza matakwa ya mkataba wa kimataifa wa Nairobi katika usimamizi na uendelezaji wa mazingira Bahari na ukanda wa Pwani katika eneo la Bahari ya Hindi kama inavyotakiwa na vyombo vingine vya Kimataifa kuandaliwa taarifa kila baada ya miaka mitano au kumi," alisema Dkt. Julius.

Alisema chapisho hilo limeandaliwa na wataalamu 18 kutoka Taasisi za Serikali na limegawanyika katika sehemu kuu sita na mandhari yake ni kuelekea uchumi wa Buluu na mchango wa rasilimali za Pwani na Bahari.

"Chapisho limebeba ujumbe mahsusi katika maeneo manne kuna viashiria vinaonesha baadhi ya makazi ya viumbe yameathirika na yapo hatarini kutoweka iwapo hatua madhubuti hazitachukuliwa ili kurejeshwa katika mazingira ya awali," alisema.

Mtaalamu huyo alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi maeneo ya Pwani na Bahari zinazotoa fursa ya kujenga uchumi wa Buluu mkubwa na endelevu kwa kuunganisha mikakati ya sekta mbalimbali.

"Chapisho hili limekuja wakati muafaka ambapo nchi yetu ipo kwenye uandaaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 na utekelezaji wa Sera na Mkakati wa uchumi wa Buluu hivyo chapisho hili ni chanzo kizuri cha taarifa za hali ya mazingira na rasilimali za Pwani na Bahari," alisema Dkt. Julius.

Kujenga uchumi wa Buluu kunahitaji mageuzi ya kimkakati katika kusimamia rasilimali za Pwani na Bahari kwa kila sekta na mageuzi yanahitaji kufanyika na yatachukua muda matokeo kuonekana.

# NEMC YAPONGEZWA KWA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MABADILIKO YA TABIANCHI



*Mratibu wa Mfuko wa Kimataifa wa kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund) Tanzania, Bw.Fredrick Mulinda (mbele) akizungmza na washiriki wa warsha iliyojumuisha Nchi 34 kwenye mkutano wa kujengeana uwezo kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya kuhimili mabadiliko ya Tabianchi katika ukumbi wa Gran Melia Jijini Arusha.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limepongezwa kwa matumizi mazuri ya fedha za miradi ya kuhimili mabadiliko ya Tabianchi kwenye mkutano wa kimataifa wa kujengeana uwezo uliozikutanisha Nchi 34 katika ukumbi wa Gran Melia Jijini Arusha.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mratibu wa Mfuko wa Kimataifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund) Tanzania, Bw.Fredrick Mulinda, alisema Nchi hizo pamoja na sekretarieti ya mfuko huo, zimepongeza na kujifunza mbinu ambazo NEMC imezitumia katika utekelezaji wa miradi na kuahidi kutumia ujuzi huo kwenye mataifa yao.

Alisema NEMC imepewa dhamana ya kusimamia fedha za kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa Tanzania kutoka kwenye mfuko huo na ilipewa uenyeji wa mkutano huo.

“Mkutano huu ulihusisha Taasisi kutoka nchi 34 ambazo zina majukumu kama ya NEMC, tumekutana Dodoma na huu ni utaratibu uliowekwa na sekretarieti ya mfuko kila mwaka kukutanisha Taasisi hizo ili kushirikishana uzoefu na ujuzi kwenye utekelezaji wa miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi,” alisema Bw. Mulinda

Alisema NEMC iliwasilisha taarifa ya miradi miwili inayotekelezwa Wilaya ya Kongwa, Bahi, Manyoni na Nzega na imejikita katika kukabiliana na ukame kwa wakulima na wafugaji.

“Wageni wametembelea Kongwa mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima na wafugaji, Mradi wa uvunaji maji kimkakati kuhimili mabadiliko ya tabianchi Bahi na baada ya hapo tulienda Arusha kwenye mkutano wa kuruhusu Taasisi zingine za mataifa mbalimbali kueleza yanayofanyika kwenye nchi zao,” alifafanua Bw. Mulinda.

Alisema mkutano huo umewezesha NEMC kuonesha Tanzania inavyokabiliana na mabadiliko hayo na umefungua fursa za utalii sambamba na kuijengea Tanzania imani kwa mfuko huo kutokana na matokeo makubwa yaliyoonekana katika miradi.

“Pia Tanzania ilipata fursa ya kufikisha ajenda ya kuharakisha mchakato wa kuidhinisha ithibati ya pili kwa NEMC kwa Adaptation Fund. NEMC imepewa dhamana ya kusimamia fedha hizi lakini kila baada ya miaka mitano huwa yanafanyika mapitio na yanapokamilika ndio hutolewa ithibati, sasa NEMC inasubiri ipate ithibati ya pili ili iombe fedha zaidi, sekretarieti imeahidi kushughulikia kwa haraka,” alisema.

Akitoa neno la ukaribisho kwenye ufunguzi wa mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Immaculate Semesi, alisema Baraza litajifunza na kubadilishana ujuzi wa kukabiliana na mabadiliko hayo ili kuendeleza jitihada hizo nchini.

“Warsha hii itakwenda kuwa chachu kwa Taifa katika mapambano dhidi ya changamoto za mabadiliko ya tabianchi,” alisema Bi. Immaculate Sware.

# NEMC, GCLA YAENDESHA MAFUNZO YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA KEMIKALI KWA MAAFISA FORODHA MPAKA WA SIRARI



*Mkurugenzi wa Huduma za udhibiti zikiwemo kemikali kutoka GCLA Bw. Daniel Ndiyo (kulia) akiwa pamoja na Meneja wa maeneo maalumu na mabadiliko ya Tabianchi NEMC Bi. Amina Kibola (kushoto) wakati wa mafunzo ya matumizi salama ya Zebaki kwa Maafisa wa Forodha.*

Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) pamoja na Ofisi ya Madini waliendesha mafunzo ya usimamizi na udhibiti wa kemikali ya Zebaki kwa Maafisa wa Forodha kutoka mpaka wa Sirari na Maafisa Mazingira kutoka Wilaya zenye shughuli za uchimbaji wa dhahabu katika Hotel ya Victoria Palace iliyopo Jijini Mwanza.

Akifungua Mafunzo hayo Mkurugenzi wa Huduma za udhibiti zikiwemo Kemikali kutoka Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Bw.Daniel Ndiyo alisema yalilenga kukumbushana wajibu uliopo kwa maafisa forodha na maafisa mazingira kwenye suala zima la usimamizi wa matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo.

Bwana Ndiyo alisema Serikali imefanya jitihada kubwa katika kuhakikisha madhara ya matumizi ya kemikali ya zebaki kwa wachimbaji yanadhibitiwa kwa kutekeleza matakwa ya Mkataba wa Minamata pamoja na kuwepo kwa Sheria zinazotoa miongozo ya utekelezaji wa matakwa ya mkataba huo ikiwemo Sheria ya Mazingira, Sheria ya Kemikali iliyopo kwa Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na Kanuni mahususi za zebaki kwa ajili ya kutekeleza mkataba huo.

Aliongeza kuwa Maafisa Mazingira kwenye Wilaya husika ndio wenye wajibu wa kusimamia masuala ya mazingira katika maeneo yao, hasa maeneo ya uchimbaji, hivyo mafunzo haya ni muhimu sana ili kuwajengea uwezo wa namna sahihi ya kuenenda katika kuhakikisha mazingira yanalindwa na kunakuwepo na matumizi salama ya zebaki kwa wachimbaji wadogo.

Naye Bi. Amina Kibola Meneja wa maeneo Maalumu na Mabadiliko ya tabianchi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) alipozungumza alisema mradi wa zebaki kwa Tanzania unatekelezwa katika Mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Shinyanga, Mbeya, Songwe na Singida huku ukiratibiwa na Baraza na jukumu la elimu kukasimiwa kwa ofisi ya maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Bi. Amina alisema malengo ya mradi ni kuimarisha taasisi husika kujenga uwezo na ujuzi katika kutekeleza matakwa ya Mkataba wa Minamata, kuwezesha mabadiliko ya kisera, pamoja na kuboresha matumizi ya teknolojia.

# ELIMU YA MATUMIZI SALAMA YA ZEBAKI YAWAFIKIA WACHIMBAJI WADOGO TAKRIBANI 600 MKOA WA MARA



*Wachimbaji wadogo wa dhahabu kutoka Kata ya Kenyamanyori Mkoa wa Mara wakifuatilia elimu ya matumizi salama ya Zebaki.*

Elimu ya matumizi salama ya zebaki kwa wachimbaji wadogo iliyotolewa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) pamoja na Ofisi ya Madini iliwafikia wachimbaji wadogo takribani 600 Mkoa wa Mara.

Elimu hiyo iliyotolewa kupitia Mradi wa kudhibiti matumizi ya Kemikali ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wanaotumia kemikali ya zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu unaofadhiliwa na Bank ya Dunia imelenga kuainisha sifa za zebaki, namna inavyoingia mwilini, madhara yatokanayo na matumizi ya zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu, namna ya kujikinga na athari pamoja na namna ya kuihifadhi.

Akitoa elimu kwa wachimbaji wadogo wa Mkoa wa Mara iliyohusisha wachimbaji kutoka machimbo ya Nyangoto, Kenyamanyori na Irasamilo, Meneja kutoka Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Bw.Musa Kuzumila alisema elimu hii ni katika kutekeleza Mkataba wa Minamata wenye takwa la kuwa na mpangokazi wa utoaji elimu ya matumizi salama ya zebaki kwa wachimbaji wadogo.



*Bw. Mussa Kuzumila Meneja kutoka Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali akitoa elimu ya matumizi Salama ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo Mkoa wa Mara.*

Alisema Zebaki madhahara yake ni kuharibu mfumo wa fahamu unaopelekea ulemavu wa viungo, Figo, kuhisi, msongo wa mawazo, ngozi kuharibika, mimba kwa wanawake kuharibika, kuzaa watoto wenye ulemavu na kupoteza nguvu za kiume.

Bwana Kuzumila pia alizitaja njia za kuzuia madhara wakati wa uchenjuaji kuwa ni kutumia vifaa kinga kama gloves, barakoa, respirator, overall, mabuti, miwani na helmet wakati wa uchenjuaji.

Aliongeza kuwa zebaki inatakiwa kuhifadhiwa vizuri kwa kuzingatia lebo kusomeka kwa lugha ya kiswahili na kingereza, isihifadhiwe nyumbani, isiwekwe karibu na tindikali, Ammonia au Metal, iwekwe kwenye kifungashio, ufuniko wa chupa ufungwe vizuri na itunzwe kwenye eneo kavu na lenye mzunguko mzuri.

# ELIMU YA MATUMIZI SALAMA YA ZEBAKI YATUA KIJIJI CHA RWAMGASA-GEITA






*Picha zikionesha washiriki wa mafunzo ya matumizi salama ya Kemikali ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wakifuatilia mada.*

Elimu ya matumizi salama ya zebaki imetolewa kwa wachimbaji wadogo walioko Kata ya Rwamgasa Kijiji Cha Lwamgasa Wilaya ya Geita vijijini Mkoa wa Geita.

Akitoa elimu hiyo yenye lengo la kujenga utambuzi wa madhara ya matumizi ya kemikali ya zebaki na namna ya kujikinga Bw. Musa Kuzumila, Meneja wa usajili wa kemikali na Maabara za Kemia kutoka ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali amesema elimu hii ni katika kutekeleza mkataba wa Minamata wenye takwa la kuandaa mpango kazi wa namna sahihi ya kudhibiti matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo.

Aliongeza kuwa matumizi yasiyo salama ya kemikali ya zebaki huleta athari za kiafya ambazo ni kuharibiwa kwa mfumo wa fahamu na viungo muhimu vya mwili hali inayopelekea kushindwa kuhisi, kukakamaa kwa mwili, macho kuharibika, kushindwa kufanya kazi, kupoteza nguvu za kiume, msongo wa mawazo, kuwashwa kwa ngozi na mwili kudhoofika,

Naye Bw. Dereki Masako, Mkemia kutoka Ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali alipozungumza alisema zebaki iko katika hali ya kimiminika kizito na ni moja kati ya vyanzo kumi vinavyohatarisha zaidi afya ya jamii kutokana na shughuli za kibinadamu

Ameongeza kuwa inauwezo wa kusafiri masafa marefu, hudumu kwa miaka mingi, hujilimbikiza katika mfumo mfuatano wa chakula na huleta madhara kwa afya na mazingira.

Bw. Dereki alisema kemikali ya zebaki huingia mwilini kwa njia ya hewa, kupitia ngozi au macho, kula au kumeza na kupitia tumbo la uzazi la Mama na kuwataka wachimbaji kutumia vifaa Kinga kama gloves, miwani, mabuti, koti, kofia, reflector, barakoa au respirator na kizimamoto ili kujikinga na athari za kiafya zinazoweza kutokea.

Naye Bwa. Zakaria Deus, Afisa Mteknolojia kutoka Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Kanda ya ziwa alipozungumza ameeleza usimamizi na uhifadhi wa zebaki kuwa uzingatie kusomeka kwa lebo ikiwa na lugha ya kiswahili na kiingereza, ihifadhiwe vizuri, isitunzwe nyumbani, ifunikwe kwenye vifungashio, itunzwe kwenye eneo kavu na lenye mzunguko mzuri na isitunzwe karibu na tindikali, Ammonia na Metal

Katika hatua nyingine Bi. Hyasinta Laurean kutoka Tume ya Madini-Geita alipohojiwa alikiri kufurahishwa na elimu ya matumizi salama ya zebaki inayoendelea na kuwataka wachimbaji wa Rwamgasa kuzingatia hilo ili kulinda afya yao na afya ya Mazingira.

# NEMC YAPIGA KAMBI KANDA YA ZIWA, ELIMU YA MATUMIZI SALAMA YA ZEBAKI YATOLEWA



*Bi. Amina Kibola Meneja wa maeneo maalumu na mabadiliko ya Tabianchi (kushoto) akiwa na Meneja wa Kanda ya Ziwa Bw. Jerome Kayombo wakati wa mafunzo ya elimu ya matumizi salama ya zebaki kwa wachimbaji wadogo.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Madini kupitia Mradi wa Zebaki unaofadhiliwa na Benki ya Dunia wametoa elimu ya matumizi sahihi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo kutoka Mgodi wa Chata, Shokeraera, Shilalo na luhala zilizopo Wilaya ya Misungwi Mkoa wa Mwanza

Akitoa elimu hiyo iliyohusisha matumizi salama ya zebaki kwa wachimbaji, Bw. Musa Kazumila Meneja wa usajili wa kemikali na maabara za kemia, kutoka ofisi ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali alisema ni kufuatia Mkataba wa Minamata (Minamata convention) unaotaka kutekeleza matakwa yake moja likiwa la kudhibiti matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo.

Bwana Kuzumila alisema katika mradi huu unaoratibiwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mkemia Mkuu amepewa jukumu la kutoa elimu ya usimamizi salama pamoja na matumizi salama ya zebaki kwani ndiye anayesimamia utekelezaji wa Sheria Na.3 ya mwaka 2003 inayohusu usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na majumbani ikiwemo zebaki.

Aidha alifafanua kuwa lengo la utoaji wa elimu hii pia ni kuwajengea uwezo wa uelewa kwa wachimbaji na watumiaji wa zebaki ili waweze kutambua jinsi zebaki inavyoingia mwilini, madhara yake na namna ya kujikinga.

Naye Bw. Dereki Masako kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Dodoma alipozungumza aliainisha maeneo ambapo madhara ya zebaki yanatokea kuwa ni wakati wa usagaji wa mawe na kudondosha matope ili zebaki ikamate na wakati wa uchukuaji wa kusanyiko anapokamua na kitambaa kwani matone hudondoka chini na kusambaa ardhini na hewani na kuleta madhara.

Alisema ni vema wachimbaji wakatumia vifaa Kinga ili kujilinda dhidi ya athari za zebaki na kubainisha madhara yake kuwa ni kuharibu mfumo wa fahamu na kuleta athari ya kushindwa kuhisi, kukakamaa kwa mwili, macho kuharibika na Figo.

Kwa mama wajawazito huathiri ukuaji wa mtoto kwa sumu kupita kwenye kondo la mama, kupoteza nguvu za kiume kwa wanaume, msongo wa mawazo na mwili kuwasha na kupungua.

Naye katibu wa Chama cha wachimbaji wadogo Wilaya ya Misungwi alipozumngumza alikiri kutokuwa na uelewa wa madhara ya zebaki na amefurahishwa na elimu hii kwani wengi wao wamekuwa wakijishughulisha na uchimbaji wa dhahabu bila kuzingatia madhara ya kiafya yanayoweza kutokea



*Bw. Mussa Kuzumila Meneja wa usajili wa Kemikali kutoka GCLA akizungumza na wachimbaji wadogo wa Shilalo –Geita.*



*Bw. Mussa Kuzumila Meneja wa usajili wa Kemikali kutoka GCLA akizungumza na wachimbaji wadogo wa Butiama.*

# WANACHAMA WA TASCC KUTOKA SHULE YA ST. MARYGORETI WAPATIWA ELIMU YA MAZINGIRA



*Afisa Mazingira mkuu NEMC Bi. Aminata Kirama (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wanachama wa Chama cha Tanzania Students Coalition on Climate (TASCC) kutoka shule ya St. Marygoreth iliyoko Moshi mkoani Kilimanjaro mara baada ya kupatiwa mafunzo ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira katika ofisi za NEMC Jijini Dar es Salaam.*

Wanachama wa Chama cha Tanzania Students Coalition on Climate (TASCC) kutoka Shule ya St. Marygoreti iliyoko Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro wamefika Ofisi za Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Jijini Dar es Salaam kupatiwa elimu juu ya masuala mazima ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira na namna Baraza linavyotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake.

Akizungumza na wanachama hao ambao ni wanafunzi kutoka kidato cha kwanza hadi cha nne, Afisa Mazingira Mkuu wa NEMC Bi. Aminatha Kirama amesema elimu iliyotolewa ni kuhusiana na masuala ya Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria, Tafiti za Mazingira pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

Bi. Aminatha ametoa rai kwa wanafunzi wa shule nyingine kutembelea Ofisi za NEMC kujifunza namna Bora ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake.

“Nitoe rai kwa wanafunzi wa shule nyingine nchini kufanya kama ambavyo umoja huu wa wanafunzi kutoka Marygoreti kuja kujifunza mengi kuhusiana na masuala ya utunzaji wa mazingira na sisi kama Baraza tupo tayari kuendelea kutoa huduma hii kwa wanafunzi.” Amesema Bi. Aminatha.

Akizungumza kwa niaba ya wanachama hao ambao pia ni wanafunzi wa Shule ya Marygoreti. Ndugu Liberata Light Livinus amesema imekuwa faida kubwa kwao kutembelea Ofisi za Baraza kwani wamepata elimu ya utunzaji wa mazingira na hivyo kuwawezesha kuwa mabalozi wazuri kwenye masuala mazima ya mazingira.

“Tumejifunza mambo mengi mazuri na hasa tumepata kujua kuwa kuna uhitaji mkubwa wa kila mwananchi na hasa sisi vijana kupambania mazingira yetu, tumejua Baraza linahitaji nini kutoka kwa vijana na vijana nini tunahitaji kutoka Baraza katika kuhakikisha mazingira yetu yanaendelea kuwa salama.” Alisema Bi. Liberata.

Akitoa rai kwa wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira Bi. Liberata amesema ni jukumu la kila mwananchi kutupa taka sehemu sahihi huku akisisitiza kutenganisha taka hizo.

“Unapokuwa na taka tupa sehemu sahihi tena kwa kuzitenganisha na hasa hospitalini ili zisichanganyike na kuleta madhara kwa jamii.” Alisisitiza Bi. Liberata.

# MAAFISA FORODHA MPAKA WA TUNDUMA NA MAAFISA MAZINGIRA WA MIKOA YA SONGWE NA MBEYA WAPATIWA MIONGOZO NA ELIMU YA MATUMIZI SALAMA YA ZEBAKI




*Bw. Boniphace Kyaruzi akitoa elimu juu ya muongozo wa uingizaji na utumiaji wa kemikali ya Zebaki kwa Maafisa forodha mpaka wa Tunduma.*

Maafisa Forodha wa mpaka wa Tunduma na Maafisa Mazingira wa Mikoa ya Mbeya na Songwe wapatiwa mafunzo juu ya Muongozo wa Uingizaji na Utumiaji wa kemikali ya Zebaki nchini.

Mafunzo hayo yalitolewa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika ofisi za mpaka wa Tunduma Mkoa wa Songwe.

Akitoa mafunzo hayo Bw. Boniface Kyaruzi Mhandisi Mazingira wa NEMC amesema ni kwa lengo la kuwajengea uelewa wa namna sahihi ya usimamizi, uingizaji halali na matumizi salama ya kemikali ya zebaki kwa wachimbaji wadogo ili kuepuka athari za kiafya na kimazingira

Bwana Kyaruzi aliongeza kuwa mafunzo haya yaliyoendeshwa kupitia Mradi wa Kudhibiti Matumizi ya Kemikali ya Zebaki (EHPMP) unaofadhiliwa na Benki Kuu ya Dunia na kuratibiwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ni mahususi kwa ajili ya utekelezaji wa maazimio ya Mkataba wa MINAMATA wenye takwa la kuandaa mpango kazi wa Kitaifa kwa kila Nchi mwanachma wa namna sahihi ya kudhibiti matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo kwa dhumuni la kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yatokanayo na uchafuzi wa zebaki.

Naye Bw. Jansen Bilaro Mkemia kutoka Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Mkoa wa Mbeya alipozungumza aliwataka Maafisa hao kushirikiana bega kwa bega na Ofisi ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika kudhibiti uingizaji haramu na matumizi yasiyo salama ya kemikali ya zebaki kwa kuhakikisha waingizaji, wasambazaji na wachimbaji wadogo wanasjiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kemikali Na.3 ya mwaka 2003 inayohusu usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na majumbani ikiwemo zebaki.

# ELIMU YA UTUNZAJI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA YATOLEWA BANDA LA NEMC MAONESHO YA MBEYA CITY EXPO 2024

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilitoa elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake kwenye maonesho ya Mbeya City Expo yaliyofanyika Jijini Mbeya.

Akizungumza na wananchi kwenye Maonesho ya Mbeya City Expo 2024, Meneja wa Kanda hiyo, Bw. Josiah Murunya, alisema NEMC inashiriki maonesho hayo na itatoa Elimu kwenye maeneo sita yakihusisha hatua za kuzingatia wakati wa kufanya Tathimini ya athari kwa Mazingira (TAM), namna ya kusajili miradi NEMC kwa kutumia mfumo kielekitoniki (PMS), katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki, namna ya kudhibiti sauti zilizozidi viwango, umuhimu wa kuzingatia elimu ya sahihi ya utunzaji wa mazingira pamoja na kusikiliza malalamiko na changamoto za kimazingira kutoka kwa wananchi na kuzitatua.

"Kauli mbiu ya maonesho hayo ni kuchochea uwekezaji na biashara kwa uchumi endelevu" ambapo NEMC itayatumia kwa kutangaza majukumu na wajibu ilionao kwenye Mazingira na kwa wananchi, wawekezaji na wafanyabiashara wanaoshiriki kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira.

"Tunajenga na kuendeleza mahusiano kati ya Baraza na Wananchi, wawekezaji, wafanyabiashara, Taasisi za Serikali na Binafsi, kujifunza mambo mapya yatakayosaidia kuboresha utoaji wa huduma zetu," alisema.

Alibainisha kuwa kumekuwapo na uelewa mdogo wa wanachi na wafanya biashara kuhusu Sheria ya Mazingira na Kanuni zake, hivyo kupitia maonesho hayo Baraza litaweza kutangaza huduma zitolewazo kwa wananchi na wadau mbalimbali wa Mazingira.

"Tunatarajia wawekezaji na wafanyabiashara wengi wenye miradi waweza kusajili miradi yao katika Baraza, Wawekezaji na wananchi wajue wajibu wao katika kutunza na kuhifadhi Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake ikiwa ni pamoja na kulipa Ada na Tozo za Mazingira kwa miradi inayofanya kazi," alisema.




*Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Bw. Josiah Murunya akitoa elimu ya Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira kwa mwananchi aliyetembelea banda la Maonesho ya Mbeya City Expo 20204.*

# NEMC YASHIRIKI MAADHIMISHO YA MAZINGIRA DUNIANI YALIYOFANYIKA KITAIFA JIJINI DODOMA KATIKA VIWANJA VYA JAKAYA KIKWETE CONVENTION CENTER




*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dr. Immaculate Sware Semesi (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa NEMC kwenye banda la maonesho siku ya uzinduzi wa wiki ya mazingira duniani katika viwanja vya Jakaya Kikwete Convention Center Dodoma.*

Tarehe 5 Juni, ya kila mwaka Watanzania wanaungana na Mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Hii ni katika kutekeleza maazimio ya Baraza la Umoja wa Mataifa la mwaka 1972, wakati wa mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa Stockholm, nchini Sweden ambapo Azimio la kuunda Shirika la Umoja wa Mataifa la kushughulikia Mazingira (UNEP) lilipitishwa siku hiyo. Kuanzia wakati huo hadi sasa Nchi mbalimbali Duniani huadhimisha siku muhimu na ujumbe maalumu wenye falsafa ya Utunzaji wa Mazingira unaotolewa na Umoja wa Mataifa. Dhumuni kuu la maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ni kuhamasisha jamii duniani kote kuelewa masuala yanayohusu mazingira na pia kuhamasisha watu wa jamii mbalimbali duniani kuwa mstari wa mbele katika kuchukua hatua za kuhifadhi na kusimamia mazingira.

Hii ni kwa sababu pamoja na kuwa na urithi wa kipekee wa maliasili na bioanuai, nchi yetu ya Tanzania imeendelea kukumbwa na athari za kimazingira zikiwemo athari za kiasili na zile zinazosababishwa na shughuli za kila siku za mwanadamu. Kwa kiasi kikubwa athari za mazingira (uharibifu na uchafuzi) zinasababishwa na kukua kwa miji, ongezeko la watu pamoja na kukua kwa shughuli za kiuchumi. Changamoto hizi zimeendelea kuhatarisha ubora wa maliasili na mazingira tuliyonayo hivyo kuathiri afya ya jamii na mifumo ya kiuchumi. Hali ya mazingira nchini imefafanuliwa kwa kina kwenye **Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032).** Mpango huo umetoa mwelekeo na vipaumbele vya namna changamoto za kimazingira nchini zinavyoweza kutatuliwa kwa ufanisi. Aidha, ili kukabiliana na changamoto za kimazingira, tunatakiwa kuchukua hatua madhubuti na mageuzi endelevu ya kiuchumi kwa kuwa maendeleo ya jamii yanategemea kwa kiasi kikubwa mipango, mikakati, na taratibu za uhifadhi na usimamizi wa mazingira na kuwaleta pamoja wadau mbalimbali wa mazingira ili kujadiliana masuala ya Mazingira na kufikia maamuzi juu ya hatua stahiki zinazopaswa kuchukuliwa katika kukabiliana na changamoto za kimazingira.

Kwa mwaka 2024 Kimataifa, maadhimisho hayo yaliyozinduliwa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Biteko na kulihutubia Taifa la Tanzania umuhimu wa Wizara na Taasisi zote kuwa na vitengo vya Mazingira kwani kila mmoja katika utekelezaji wa majukumu ya Umma anagusa Mazingira yalifanyika Dodoma katika viwanja vya Jakaya Kikwete Convention Centre kwa kauli mbiu ya kidunia isemayo “Urejeshwaji wa Ardhi, ustahimilivu wa hali ya jangwa na ukame”, ambapo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kama chombo kilichokasimiwa madaraka ya kusimamia na kuhifadhi Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake na chenye wajibu wa kuishauri Serikali namna bora ya kutunza mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa kilishiriki kikamilifu kwenye maonesho ya Mazingira mwaka huu kwa kutoa elimu kwa umma juu ya Umuhimu wa kusimamia na kuhifadhi Mazingira kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira, Umuhimu wa Ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Umuhimu wa ufanyaji wa kaguzi za Mazingira kwenye miradi iliyopatiwa vyeti, Athari za sauti zilizozidi viwango pamoja na katazo la matumizi ya mifuko ya Plastiki.

Kwa kipindi chote cha maonesho ya wiki ya mazingira , Baraza kupitia wataalamu wa Mazingira lilifanikiwa kukutana na wananchi ana kwa ana na kujadiliana namna bora ya kuhifadhi na kusimamia mazingira na kukusanya maoni kutoka kwa wadau ikiwa ni pamoja na kugawa machapisho mbalimbali yenye jumbe tofauti tofauti za Mazingira.

Katika maadhimisho hayo yalioambatana na mfululizo wa Shughuli za Kimazingira kwa wiki nzima zilizohusisha usafi na uzinduzi wa matukio muhimu, yalilenga kutoa elimu ya mazingira ikiwa ni pamoja na kuinua msukumo au chachu au utamaduni wa kuyajua mazingira, kuyahifadhi na kuyasimamia kwa Mujibu wa Sheria ya Mazingira na kwa maendeleo endelevu ya Taifa. Sambamba na hayo , Baraza lilishiriki katika shughuli zilizoandaliwa na ilizoandaa kama sehemu ya Maadhimisho ya wiki ya Mazingira Duniani. Shughuli hizo ni pamoja na;

Uzinduzi wa mradi wa urejeshaji wa

uoto wa asili unatekelezwa katika Wilaya saba (7) na Mikoa mitano ambayo ni Iringa, Njombe, Rukwa, Mbeya na Katavi. Uzinduzi wake ulifanywa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Seleman Jafo kwa kuzindua josho la Mifugo na ugawaji wa hati miliki za kimila na hati za misitu 4450 Mkoani Katavi.

Kongamano la Mazingira lilioratibiwa na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) tarehe 31 Mei mwaka huu katika kituo cha Kimataifa cha mikutano cha JNICC Dar es Salaam lililohusisha washiriki takribani 1,200 kutoka Mikoa mbalimbali hapa Nchini, Mabalozi kutoka mataifa ya uwakilishi hapa Nchini, wadau wa Mazingira, Wizara, sekta binafsi na za Serikali, Taasisi za Serikali na binafsi, Vyuo vikuu, mashirika binafsi na ya Serikali, Wizara na Halmashauri zote, pamoja na Asasi za kiraia kwa lengo la kujadiliana namna bora ya kusimamia na kuhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu ya Taifa. Mgeni rasmi katika kongamano hilo alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango ambapo katika hotuba yake alisisitiza masuala ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye Sheria ya Mazingira na machapisho ya Mazigira ili kuweza kuwafikia wananchi wengi hasa wale wa ngazi ya chini kabisa.

Tarehe 01 Juni mwaka huu kulifanyika zoezi la usafi nchi nzima ambapo viongozi wa Serikali waliongoza watanzania katika Mikoa na Wilaya walizopangiwa kufanya usafi wa Mazingira. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam zoezi liliongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango kwa kufanya usafi katika Soko la Ilala. Katika hotuba yake alisema lengo la kufanya usafi ni kuamsha ari ya watanzania kuona umuhimu wa kutunza Mazingira katika kila siku na sio kusubiri matukio muhimu.

Tarehe 03 Juni mwaka huu, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko alizindua mabanda 46 ya maonesho katika viwanja vya Jakaya Kikwete convention Centre Dodoma. Katika Hotuba yake baada ya uzinduzi alizitaka mamlaka za



*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko(Kushoto) alipozuru Banda la NEMC uzinduzi wa maonesho ya wiki ya Mazingira Duniani katika viwanja vya Jakaya Kikwete Convention Dodoma (Katikati) Ni waziri mwenye dhamana na Mazingira Mhe. Dkt. Seleman Jafo.*

Serikali zote na Wizara kuhakikisha wanakuwa na kitengo cha Mazingira ili kwa pamoja yaweze kuhifadhiwa na kulindwa. Alilitaka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuhakikisha wanaweka mikakati ya namna ya kuhifadhi Mazingira na sio kutumia nguvu nyingi na Sheria hali inayowafanya wananchi kuwa na uoga.

Naye Waziri mwenye dhamana ya Mazingira Mhe. Dkt Seleman Jafo alipozungumza alisisitiza umuhimu wa kutumia nishati safi ili kutunza Mazingira

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko(Kushoto) alipozuru Banda la NEMC uzinduzi wa maonesho ya wiki ya Mazingira Duniani katika viwanja vya Jakaya Kikwete Convention Dodoma (Katikati) Ni waziri mwenye dhamana na Mazingira Mhe. Dkt. Seleman Jafo.

Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani kilifanyika Jijini Dodoma katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre. Mgeni rasmi siku hiyo alikuwa Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango. Katika hotuba yake alizungumza yafuatayo:- Hali halisi ya uharibifu wa mazingira nchini, hasa kiwango cha upotevu wa maeneo ya misitu kuongezeka kutoka hekta 378,160,000 mwaka 2019 hadi kufikia hekta 469,420,000, kwa mwaka 2023, kiwango cha matumizi ya kuni na mkaa kimeongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na idadi ya watu, kwa sababu hiyo Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amejitoa kuwa kinara wa nishati safi ya kupikia.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango (katikati) pamoja na viongozi mbalimbali wa Serikali wakiwa katika picha ya pamoja na Menejiment ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) pamoja na Menejimenti ya Baraza mara baada ya kulihutubia Taifa siku ya kilele cha mazingira tarehe 05/06/2024

Makamu wa Rais Pia alieleza mpango wa Serikali wa kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaojumuisha kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya mazingira ya mwaka 2021, mpango kabambe wa Taifa wa Hifadhi na usimamizi wa mazingira wa mwaka 2022 hadi 2032 na kuongeza kasi ya upimaji na umilikishaji wa ardhi kimila na uhamasishaji wa matumizi endelevu ya Ardhi hususanu kilimo mseto, kilimo cha matuta, kilimo hifadhi na mbinu endelevu za kiasili za hifadhi ya malisho.

Katika maadhimisho hayo pia kulizinduliwa Sera ya Taifa ya uchumi wa buluu ya mwaka 2024 na Mkakati wa utekelezaji wa sera hiyo kwa kipindi cha mwaka 2024 hadi 2034. Sera hii ni muhimu kwa kuwa uchumi wa buluu ni dhana inayohimiza ukuaji wa uchumi kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za maji pamoja na kudhibiti uchafuzi wa bahari maziwa na rasilimali nyingine.

# NEMC YAWAONYA WAUZAJI CHUMA CHAKAVU KUHUSIANA NA ATHARI KIAFYA



*Bw. Edgar Mugila Meneja wa Kanda ya Magharibi akiongea na wauzaji wa chuma chakavu katika zoezi la utoaji elimu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira inayoendelea katika Kanda hiyo.*

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Magharibi limewatahadharisha wauzaji wa chuma chakavu juu ya uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli zao hali inayohatarisha afya za binadamu na kuathiri mazingira.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha utoaji elimu wa kuhifadhi na kusimamia Mazingira kilichofanyika Wilaya ya Igunga, Meneja wa Kanda inayojumuisha Mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi, Bw. Edgar Mgila, alisema wafanyabiashara wa chuma chakavu hawafuati Sheria katika kuhifadhi mazingira wakati wa utekelezaji wa shughuli zao, bali wanahifadhi kwenye maeneo ambayo si salama hayajasakafiwa wala kuezekwa.

“Kwa mfano eneo halina sakafu na wala halijafunikwa juu ni rahisi wakati wa mvua kutiririsha sumu ya chuma inayoweza kusababisha madhara kwenye jamii,” alifafanua Bw. Edgar.

“Jukumu letu ni kufanya kaguzi na kutoa elimu kwa wadau na kutoa maelekezo tunapofanya kaguzi, kwa kipindi cha mwezi Mei tumefanya ukaguzi Wilaya ya Igunga na Nzega na kutoa elimu ya usimamizi wa mazingira,” alisema.

Alisisitiza kuwa zoezi hilo kutokana na hali hiyo, imeanza kufanya ukaguzi na kutoa elimu kwa wafanyabiashara hao na wachimbaji madini ili kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mazingira na Kanuni ya usimamizi wa mazingira ya taka hatarishi na taka za kielekroniki za mwaka 2021na linaendelea kwenye maeneo mengine ya kanda hiyo ili kunusuru afya za wafanyabishara wa vyuma chakavu na wachimbaji.

Naye, Diwani wa Kata ya Nguvumoja, Alferd Nkuba, alipongeza NEMC kwa kutoa elimu hiyo kwa wachimbaji kuhusu sheria ya mazingira na kanuni zake ili wazingatie usalama wa afya zao na uhifadhi wa mazingira.

Nao, viongozi wa wafanyabiashara ya chuma chakavu, Bw. Boaz Dhahabu na Idaso Mayanda walipendekeza vibali vya chuma chakavu vitolewe kwa wafanyabishara kulingana na mitaji yao ili kukidhi matakwa ya Kanuni.

# WAZIRI JAFO MGENI RASMI HAFLA YA KUWAAGA WASTAAFU NEMC

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo alimshukuru Dkt. Samuel Gwamaka Mafwenga kwa kuwa msaada mkubwa katika kufanikisha majukumu yake kama Wiziri mwenye dhamana ya Mazingira alipoteuliwa kushika wadhfa huo.

Waziri Jafo aliyasema hayo Aprili 27 mwaka huu alipokuwa akizungumza na Wafanyakazi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) katika hafla ya kuwaaga wastaafu Dkt. Samweli Mafwenga aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Baraza na Bw. Lewis Nzali aliyekuwa Meneja wa Kanda ya Kaskazini pamoja na Bw. Anold Kisiraga Afisa wa NEMC hafla iliyofanyika katika Hotel ya Serena Jijini Dar es Salaam

Waziri Jafo alisema kuwa alipoingia kwenye Wizara hiyo hakuwa anafahamu mengi kuhusu mazingira lakini kutokana na uwepo wa Dkt. Gwamaka aliweza kutekeleza majukumu yake kwa urahisi.

"Nilikuja Ofisi ya Makamu wa Rais nikiwa sijui mengi kuhusiana na Mazingira lakini ninyi kwa umoja wenu mkiongozwa na Dkt. Gwamaka mmenitengeneza nimeweza kuyajua Mazingira japo sio kwa asilimia zote lakini kwa kiwango cha kuridhisha nimeweza kujua masuala ya Mazingira." Alisema Waziri Jafo.

Waziri Jafo aliongeza kuwa wakati anaanza kuitumikia Wizara yenye dhamana ya Mazingira alikuta Dkt. Gwamaka anamaliza muda wake lakini alimuombea ili aweze kuendelea na kazi ambapo ombi hilo lilikubaliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Dkt. Gwamaka akaongezewa muda wa kuendelea kulitumikia Baraza.

Akitoa salamu kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhandisi Cyprian Luhemeja, Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Bi. Christina Mndeme aliwapongeza wastaafu hao na kusifu utendaji kazi wa Dkt. Gwamaka.

"Kwakweli tunaufurahia, tunauenzi, tunauamini na tunauthamini utendaji wako na umeacha alama kwenye Baraza na hata hii mifuko ya plastiki tulijiuliza kama tutaweza lakini tuliweza kwa sababu ulitoka na ulisema." Alisema Bi. Christina.

Akitoa neno kwenye hafla hiyo Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi NEMC Mhandisi Profesa Esnat Chaggu amesema wakati wanaanza kutekeleza Majukumu yao walikuta malalamiko mengi sana lakini kwa kushirikiana na Dkt. Samuel Gwamaka waliweza kuyapunguza kwa kiasi kikubwa.

"Tunashukuru kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mkuu tuliweza kupunguza malalamiko kwa kiasi kikubwa kwani alijitahidi na kupambana kurekebisha ofisini na mtaani kila mahali kuhakikisha kwamba malalamiko yanapungua, naishukuru pia Bodi ya Wakurugenzi NEMC kwani walikuwa tayari muda wote kumpa ushirikiano usiku na mchana." Alisema Profesa Chaggu.

Kwa upande wake Dkt. Gwamaka aliwashukuru Wafanyakazi wa Baraza na kuwaomba kumpatia ushirikiano Mkurugenzi Mkuu mpya wa Baraza Dkt. Immaculate Sware Semesi kama ambavyo wamempatia yeye kipindi akitekeleza Majukumu yake kama Mkurugenzi Mkuu wa Baraza.

Aidha aliwatia moyo wafanyakazi hao wa Baraza kwani kazi wanayoifanya ni njema sana licha ya kuwa ni ngumu na wakati mwingine hata kuhatarisha maisha yao wakiwa katika kutekeleza Majukumu yao.



*Picha ikimuonesha Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt Seleman Jafo (wapili kushoto) akifurahia jambo na viongozi mbalimbali wakati wa hafla ya kuwaaga wastaafu. (wa kwanza kushoto) ni Mkurugenzi Mkuu NEMC Dkt. Immaculate S. Semesi, na (wa kwanza kulia) ni Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) Bi. Christina Mndeme.*

# WAZIRI JAFO AWATAKA MAAFISA MAZINGIRA NCHINI KUSIMAMIA SHERIA YA MAZINGIRA KWENYE MAENEO YAO



*Bw. Boniphace Kyaruzi akitoa elimu juu ya muongozo wa uingizaji na utumiaji wa kemikali ya Zebaki kwa Maafisa forodha mpaka wa Tunduma.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo aliwaelekeza maafisa mazingira katika Halmashauri zote nchini kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 katika maeneo yao.

Waziri Jafo aliyasema hayo wakati wa kikao na mameneja wa Kanda wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Aprili 18, mwaka huu Jijini Dodoma.

Alisema Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 imeainisha wazi kuwa maafisa hao wanapaswa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu yao ya usimamizi wa mazingira kwa Mkurugenzi wa Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais na NEMC kwa ajili ya ufuatiliaji.

“Niwatake maafisa Mazingira wote nchini wa Serikali za mitaa na kwenye Taasisi mbalimbali wahakikishe kuwa wanasimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika maeneo yao ili kuisaidia Nchi yetu katika kutunza mazingira” Alisema Waziri Jafo.

Aidha, kutokana na changamoto mbalimbali za kimazingira hususani kelele na mitetemo, Dkt. Jafo alizielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuishirikisha Ofisi ya Makamu wa Rais katika upangaji wa miji ili kuondoa changamoto ya kelele katika maeneo ya makazi.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mwongozo wa Udhibiti wa Kelele na Mitetemo ya mwaka 2021 kwa kipindi cha miaka miwili Mkurugenzi wa Utekelezaji na Uzingatiaji wa Sheria NEMC Dkt. Thobias Mwesiga alisema kuwa elimu imeendelea kutolewa na malalamiko yanapokelewa na hatua zimeendelea kuchukuliwa.

“Baraza limeendelea kupokea malalamiko yanayohusu kelele chafuzi za mazingira kutoka kwa wananchi na kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo za kufanya kaguzi eneo husika kujiridhisha kwa kuchukua vipimo, kuwaita walalamikiwa kuwasikiliza na kuwapa maelekezo na kutoa adhabu stahiki kwa mujibu wa Sheria.” Alisema Dkt. Mwesiga.

# NEMC KUSHIRIKIANA NA PEW NA WETLANDS INTERNATIONAL KATIKA UHIFADHI WA MAENEO YA FUKWE ZA BAHARI

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa yasiyo ya kiserikali ya Pew Charitable Trusts (PEW) na Wetlands International (WI) wajipanga kuhifadhi maeneo ya fukwe za bahari.

Hayo yalibainishwa Aprili 17 Mwaka huu katika mkutano wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dkt. Selemani Jafo na Wakurugenzi wa Mashirika ya Kimataifa yasiyo ya Kiserikali ya The Pew Charitable Trusts (PEW) Ndg. Simon Redds na Wetlands International (WI) Bi. Julie Mulonga pamoja na timu ya wataalamu walioambatana nao kwa lengo la kuanisha fursa zilizopo kwenye uhifadhi wa maeneo ya fukwe za bahari ikiwa ni pamoja na mifumo ya ikolojia ya mikoko na nyasi bahari (sea grass) kwa faida za kutunza bionuai na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Seleman Jafo (Katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa PEW Bw. Simon Redds (kulia kwake), Mkurugenzi wa wetland International Bi. Julie Mulonga (kushoto kwake), Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate S. Semesi (wa nne kutoka kushoto) pamoja na washiriki wa mkutano wa kuhifadhi fukwe za bahari uliofanyika Jijini Dodoma*

Waziri Jafo alipozungumza alishukuru na kueleza utayari wa Serikali katika kushirikiana nao na kubainisha kuwa taarifa za kitafiti zitakazotokana na mradi huo zitasaidia katika maandalizi ya taarifa ya Nchi kuhusu mchango wa kitaifa wa kupunguza viwango vya gesi joto duniani.

Mkutano huo ulifanyika katika Ofisi za Baraza jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mkurugenzi wa Tafiti za Mazingira NEMC Dkt. Menan Jangu na wataalamu wa Baraza.

# MIZAMBARAU 3000 YAPANDWA MTO TEGETA



*Bw. Fredrik Ugolole kwa niaba ya Meneja wa Kanda ya Mashariki Kaskazini akipanda miti ya mizambarau katika mto Tegeta, hafla ya upandaji miti iliyoratibiwa na JMAT kwa lengo la kuimarisha mazingira ya vyanzo vya maji Kata ya Goba.*

Miti 3000 aina ya mizambarau imepandwa MtoTegeta uliopo Kata ya Goba Wilaya ya Ubungo Mkoa wa Dar es salaam.

Miti hiyo ilipandwa Aprili 17,mwaka huu na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Jumuia ya Maridhiano (JMAT) kwa lengo la kuimarisha mazingira ya vyanzo vya maji ili kudhibiti mafuriko yanayotokea na kusababisha maafa katika jamii.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo, Katibu Tawala wa Wilaya ya Ubungo Bi. Beatrice Mbawala alisema miti hiyo itasaidia kudhibiti janga la mafuriko linaloweza kutokea kwa sababu ya kutanuka kwa mto Tegeta.

Naye Kaimu Meneja (NEMC) Kanda ya Mashariki Kaskazini, Bw. Andrew Ugolole alipozungumza aliwasisitiza wananchi wote kuiga mfano wa Jumuia ya Maridhiano ya Amani (JMAT) kwa kupanda miti kwa wingi hasa msimu wa mvua ili kutunza mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.




*Wasiliana nasi;*

**Mkurugenzi Mkuu,**

**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**

Ghorofa ya 6, Jengo la Kambarage, Barabara ya PSPF S.L.P 2724, Dodoma, Tanzania.

Simu: +255 26 296 0098, +255 713 608 930

Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www. nemc.or.tz


**#MazingiraYetuUhaiWetu**

Namba ya Bure: **0800110116**

@nemctanzania

NemcTVTanzania

www.nemc.or.tz

@nemctanzania